Cour
Pénale
Internationale

International
Criminal
Court

# Maulizo na Majibu

**Hali katika Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo**

Maandishi ya sasa: Mwezi wa kumi na moja

*Mwendeshamashtaka v. Bosco Ntaganda*

## Azabu katika kesi ya Ntaganda,
## Tarehe 7 mwezi wa kumi na moja 2019

### CHUMBA KILIAMUA NINI LEO?

Tarehe 7 Mwezi wa kumi na moja 2019, Chumba cha kesi cha VI cha Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (CPI) kilitoa uamuzi wa kumuazibu Bosco Ntaganda kwa miaka 30 ya kifungo. Wakati ambao Bw. Ntaganda alipitisha kwa tawi la zuizi la CPI - tangu tarehe 22 Mwezi wa tatu 2013 mpaka tarehe 7 Mwezi wa kumi na moja 2019 – utaondolewa kwa hii muda ya azabu ya kifungo.

Tarehe 8 mwezi wa saba 2019, Chumba cha kesi VI kilimpata Bw. Bosco Ntaganda na makosa ya mashtaka 18 ya makosa ya jinai ya vitani na makosa ya jinai ya binadamu, yaliyotendeka Ituri, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo (RDC) mu 2002-2003.

### UAMUZI UNAWEZA KUPIGIWA RUFAA AO KUPITIWA UPYA?

Ndiyo, utetezi na Ofisi ya Mwendeshamashtaka wanaweza kupiga rufaa kwa hii uamuzi mbele siku 30 zipite, wakichugua msingi waukosefu wa usawa kati ya kosa la jinai na azabu ya kifungo.

Tena, kufuatana na Ibara 110(3) cha Mkataba, "ikiwa mtu ametumikia mbili ya tatu (2/3) ya azabu yake ; […] Mahakama itapita upya azabu hiyo ili kuamua kama uwezekano wa kuipunguza".

### MAJAJI WALIZINGATIA NINI KWA KUTOA HII UAMUZI ?

Kwa kutoa uamzi wake, Chumba kilipokea maoni kutoka ngambo zote na pia kutoka kwa ngambo zinazoshiriki kwa kesi , kuhusu azabu. Chumba kilisikiliza mashahidi na kilipokea alama za ushuhuda, na pia kilisimamia mkutano wa watu wote kuhusu ile swala, tarehe 17, 18 na 20 ya mwezi wa kenda 2019.

Chumba kiliangalia uzito wa makosa ya jinai tofauti na aina ya hasara ambayo kila kosa ilitoa, na pia hatia ya Bw. Ntaganda, ni kusema kiasi cha nia na kushirikiana kwake. Tena, Chumba kiliangalia alama ambazo zinaongeza ukali wa maneno , kama vile tabia mbaya ya kipekee juu ya waviktime wamojamoja ambayo ilipatikana ndani ya makossa ya jinai mbalimbali.

Chumba kiliangalia hali kama vile miaka ya Bw. Ntaganda, madaraka na mafunzo aliyopata kwa kazi ya kijeshi na ujuzi wake; ujuzi wa Bw. Ntaganda wakati wa mauwaji ya kimbari (génocide) ya Rwanda; mipango ambayo inawaziwa Bw. Ntaganda alikamata kwa kulinda maisha ya maadui wapiganaji (combattants) na ya kulinda wa civils; kazi ambayo inazaniwa Bw. Ntaganda alifanya kwa kuleta amani, masikilizano na usalama Ituri mu mwaka 2004, na hali za jamaa ya Bw. Ntaganda, hali ya uzuizi wake na kujitoa mwenyewe ku Mahakama, na pia maneno alitamka kuhusu waviktime. Lakini Chumba ilivumbua ya kama kulikuwa hali za kuwatuma wapunguze ukali wa azabu. Laikini hali zile zilikosa uzito, na kufuatana na alama za ushuhuda ambazo Chumba ilipokea, hazikuangaliliwa kwa kupima huko na kule. Kwa hiyo Chumba haikuzipatia maana.

Chumba kiliangalia pia kwa jumla hali za kuongeza ukali ya maneno ambazo Ofisi ya Mwendeshamashtaka na mmoja kati ya wasimamizi ya waviktime kwa kisheria walisema. Ni kusema hali za kuwazia kama mashahidi walikuwa wanashawishiwa. Lakini Chumba hakikuzingalia hayo maoni kwa sababu hakikuona alama za ushuhuda kuhusu kushawishi mashahidi ambazo zinaheshimia kanuni ya msingi kuhusu maneno ya kuongeza ukali, hakikuona alama za ushuhuda ya bila shaka.

Katika uzibiti wake wa jumla, Chumba kilitoa azabu ya kipekee kwa kila kosa la jinai ambalo lilitendewa na Bw. Ntaganda. Azibu zile zinaanzia kwa miaka 8 mpaka miaka 30 ya kifungo.

Chumba kiliona tena ya kama makosa ya jinai ambayo Bw. Ntaganda alihukumiwa, hata kama wanajua uzito wao na kiasi ya kupatikana na makosa yake, hayakutosha kwa kuamua apewe azabu ya kifungo ya maisha mzima. Mkataba wa Roma unasema kama mtu hapewe azabu ya kifungo ya maisha, atapewa miaka 30 ya kifungo. Wakati Chumba kilitayarisha uamuzi wa pamoja kuhusu azabu ya kifungo, Chumba kiliona ya kama hakina madaraka ya kipekee ya kubadirisha kanuni ya Mkataba hapa. Kwa hiyo Chumba kiliamua kumhazibu Bosco Ntaganda kwa kifungo cha miaka 30. Kwa mwisho, wakati Chumba kiliangalia aina na ukali wa makosa ya jinai, na pia uwezo wa pesa wa Bw. Ntaganda, Chumba hakikuona ya kama ni lazima kuamua alipe amande ao malipo ingine, na kuongeza azabu ya kifungo .

## ATAFUNGIWA WAPI?

Wakati mkutano wa kusoma uamuzi wa kumpatia Bw.Ntaganda azibu unamalizika, hatabaki tena kwa Kituo cha zuizi (*Centre de detention*) ya CPI. Kufuatana na Mkataba na Kanuni za ushuhuda na utaratibu, Ofisi ya Prezidenti wa CPI, kiisha kusikiliza maoni ya mtu aliyepewa azibu, itachagua nchi moja kati ya nchi ambazo zilikubali kumpokea mtu aliyeazibiwa na inchi ambazo zilisaini makubaliano na Mahakama kuhusu hii azabu.

## WAVIKTIME WATAPATA REPARATIONS?

Waviktime mbele ya CPI wanaweza kushiriki wakati wote wa kesi. Kwa hiyo, Chumba cha kesi cha VI kiliruhusu waviktime 2.129 kushiriki kwa kesi, wakisimamiwa na wasimamizi wao wa kisheria. Bi Sarah Pellet na Bw. Dmytro Suprun ambao wanafanya kazi kwa Ofisi ya Kusimamia waviktime kwa kisheria (OPCV) ya CPI. Hata kama waviktime wanashiriki kwa kesi, wanaweza pia kuomba *réparations* kama mshtakiwa anahukumiwa. Katika iyi kesi ya Bw. Ntaganda, maneno kuhusu utaratibu wa *réparations* juu ya waviktime yatafuata wakati itakayofaa.

**www.icc-cpi.int** | Ceci n'est pas un document officiel, il est destiné à l'information du public.
Cour pénale internationale : Oude Waalsdorperweg 10, 2597 AK, La Haye, Pays-Bas. Adresse postale : Boîte postale 19519 ; 2500 CM, La Haye (Pays-Bas). Tél. + 31 (0)70 515 8515 ; Télécopie +31 (0)70 515 8555. Chaîne sur Youtube : www.youtube.com/IntlCriminalCourt ; compte Twitter : www.twitter.com/IntlCrimCourt | Flickr: www.flickr.com/photos/icc-cpi